



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT

Jaime Alicea, Superintendent of Schools

Ofisi ya Msimamizi

4 Mei 2020

Wapendwa Familia za SCSD:

Nilitaka kuwashukuru tena kwa uvumilivu, uelewa na usaidizi wenu tunapoendelea kushirikiana nyakati hizi ambazo hazijawahi kutokea. Ninajua kuwa masomo ya mbali hayajawa rahisi lakini walimu, wasimamizi na wafanyakazi wetu wanajitahidi sana kuhakikisha kuwa wewe na watoto wako mna nyenzo na usaidizi ili kufaulu kwa suala hili.

Mnapaswa kuwa mmepokea kadi ya ripoti ya kipindi cha tatu cha kusahihisha katika barua pepe. Ikiwa mtoto wako alipokea I-Incomplete ya alama ya kozi katika kipindi cha tatu cha kusahihisha, ana hadi tarehe 29 Mei, 2020 kurejesha kazi yoyote inayohitajika ili kuimarisha alama yake kutoka I-Incomplete had kiwango cha kupita. Ikiwa kuna hali zinazomzuia mtoto wako kuingia kwenye kazi yake kukamilisha kufikia makataa ya tarehe 29 Mei, tafadhali wasiliana na mwalimu wake moja kwa moja na uunde mpango wa kuongeza muda.

Taratibu za kupanga alama za robo ya nne kwa wanafunzi wetu wa msingi katika madaraja PK-5 zitawaruhusu wanafunzi kuendelea kupokea kadi za ripoti zenye alama kwa kutumia mfumo wa sasa. Tumeongeza chaguo la walimu kutoa NI-Not Enough Information, pamoja na maoni kutoka kwa walimu.

Wanafunzi wa sekondari walio katika madaraja ya 6-12 watapokea alama ya tarakimu ya kawaida (0-100) au (Incomplete) kwa kazi zilizokamilishwa katika kipindi cha nne cha kusahihisha. Alama ya mwisho ya kozi itakuwa moja ya vitu vitatu: PD (Pass with Distinction), P (Pass) au I (Incomplete). PD ni ya wanafunzi wenye alama ya tarakimu ya 85-100, P ni ya wanafunzi wenye 65-84 na I ni ya wale wenye 64 au chini. Wanafunzi wanaopata PD au P kwa alama za kozi za mwisho watapokea alama ya kozi.

Wanafunzi wanaopokea Incomplete watapendekezwa kwa shule ya majira ya joto ili kupata alama. Wanafunzi hawa pia watapewa kila nafasi na usaidizi unaowezekana kuwasilisha kazi majira ya joto ili kupata alama ya kupita ya mwaka wa masomo wa 2019-20. Machaguo ya kufidia alama ya ziada na usaidizi vitazingatiwa kwa mwaka wa shule unaofuata inavyohitajika, hadi Januari 2021.

Mitihani yote ya Regents, ikiwemo mitihani ya Agosti imefutuliwa mbali kwa mwaka wa masomo wa 2019-2020. Mwanafunzi yeyote anayefanya kozi ya Regents ambaye atapita kozi atapokea alama ya Regents.

Asanteni tena kwa kila kitu mnachokifanya ili kuwasaidia watoto wenu. Ikiwa una swali lolote kuhusu maendeleo au alama za mtoto wako, tafadhali wasiliana na mwalimu wake au mwalimu mkuu wa shule.

Wako Mwaminifu,

Jaime Alicea
Msimamizi wa Shule